JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO

MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO 2011/2012-2015/16
KUFUNGULIA FURSA FICHE ZA UKUAJI UCHUMI WA TANZANIA
MKUTANO WA MWAKA WA MAJADILIANO YA KISERA
26 HADI 27. JANUARI. 2012. DAR ES SALAAM



MPANGILIO WA MADA

1.0 Utangulizi
2.0 Sifa Mahsusi za Mpango
3.0 Mahitaji ya Msingi ya Mpango
4.0 Vipaumbele vya Mpango
5.0 Maeneo ya Uwekezaji ya Mpango
6.0 Ugharamiaji wa Mpango
7.0 Mpango na Programme nyingine za Kitaifa
8.0 Mfumo wa Utekelezaji
9.0 Viashiria vya malengo ya DIRA 2025
10.0 Hitimisho

1.0 UTANGULIZI

- Maendeleo ya nchi kwa siku za baadaye ni matokeo ya mipango ya sasa
- Mpango ni muhimu sana kwa kuwa rasilimali ni chache na mahitaji ni mengi, lazima kuchagua nini kianze na nini kisubiri, *"Kupanga ni Kuchagua"* (Mwl. J. K. Nyerere).
- Nchi kukosa Mipango ya Maendeleo ni sawa na kujenga nyumba bila ramani. Itafananaje? Gharama? Itakamilika lini? Itakidhi mahitaji?

Utangulizi, inaendelea...

- Mpango wa Maendeleo (2011/12 – 2015/16) una sehemu, tano;
  - Utangulizi
  - Mapitio ya hali ya Uchumi Jumla, Maendeleo ya Rasilimali Watu na upatikanaji wa huduma za jamii na utawala bora
  - Hatua za Kimkakati
  - Rasilimali zinazohitajika
  - Mfumo wa Utekelezaji

Dhana: *Kufungulia fursa fiche za ukuaji uchumi*

Utangulizi, inaendelea...

- Tamko la Mpango lilitolewa rasmi na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni, 2011na kupitishwa na Bunge Juni, 2011.

- Mpango Elekezi wa miaka 15 (2011/12 – 2025/26) utapitia hatua kuu tatu: **Mpango wa Kwanza (2012/12 – 2015/16);** "*kufungulia fursa fiche kwa ukuaji wa uchumi*". **Mpango wa Pili (2016/17 – 2020/21)** " *Ujenzi wa mazingira ya maendeleo ya Viwanda*". **Mpango wa Tatu (2021/22 – 2025/26)**

  "*Kuimarisha ubunifu na ushindani Kimataifa*"

Utangulizi, inaendelea ...

- Mpango umezingatia mapitio ya DIRA ya Maendeleo ya Taifa 2025, MKUKUTA II, sera na mikakati ya sekta, mikoa, wilaya na maoni ya wadau
- Tanzania imekuwa na historia ya mipango ya maendeleo (1961-1964, 1964 – 1980(1964-1969, 1969-1974, 1975-1980) na 1981-2000) na mipango ya dharura za kunusuru uchumi (1973 – 1992)
- Mipango ilikumbwa na changamoto nyingi zikiwemo kupanda kwa gharama za mafuta, kupungua kwa uzalishaji wa kilimo, vita ya Iddi Amin na mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi na kijamii.

Utangulizi, inaendelea...

- **Fursa za Tanzania**
  - Nchi ya 31 kwa ukubwa duniani (km za mraba 956,000)
  - Ardhi inayofaa kwa kilimo (Ha. 44 milioni - zinayotumika ni 24% tu); Misitu hekata 35.3 milioni; Maji eneo kubwa (km za mraba 62,000); Vyanzo vingi vya maji (bahari, maziwa na mito)vinavyofaa kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya mifugo
  - Vyanzo vingi vya kuzalisha nishati (makaa ya mawe, Umeme wa nguvu za maji, urani, upepo, jua na mawimbi ya bahari n.k.)

Utangulizi, inaendelea...

- Madini (phosphate, gesi asilia, chokaa, dhahabu, almasi, tanzanite, rubi, nikeli, bati, magadi, chuma n.k.)
- Mifugo (ng'ombe 19.2 milioni, mbuzi 13.7 milioni, kondoo 13.6 milioni n.k.)
- Fursa za kipekee kijiografia (nchi 6 jirani zisizo na mlango wa bahari; bandari nyingi za asili kwenye bahari ya hindi na bandari nyingi kwenye maziwa; ukaribu na soko kubwa la nchi za bara la Asia; mwanachama wa EAC na SADC n.k.).
- Vivutio vya kitalii (mlima Kilimanjaro, hifadhi za Taifa 15, mbuga za wanyama n.k.).

Utangulizi, inaendelea...

- **Vizuizi vya fursa za maendeleo**
  - Miundombinu
    - Nishati isiyotosheleza mahitaji ya soko
    - Uwezo na ufanisi wa bandari
    - Uchakavu wa reli
    - Ubora wa viwanja vya ndege
    - Ukosefu wa barabara kuunganisha sehemu za uzalishaji (kilimo)

Utangulizi, inaendelea...

- **Kilimo na Viwanda:**
  - Tija ndogo
  - Upatikanaji wa mikopo
  - Masoko duni
  - Uthamanishaji mdogo
  - Uwekezaji mdogo
  - Upatikanaji wa ardhi
- **Rasilimali Watu:**
  - Uhaba mkubwa wa rasilimali watu yenye ujuzi
  - Kutofanya kazi kwa bidii
  - Utegemezi wa fikra

2.0 SIFA MAHSUSI ZA MPANGO

Sifa nne (4):

- Kuondokana na utaratibu wa kupanga kukidhi mahitaji ya muda mfupi, ambayo huzingatia upeo wa rasilimali fedha inayoweza kupatikana na badala yake unaweka mfumo wa kupanga kwa kuzingatia fursa za kimaendeleo.
- Kuondokana na ubainishaji wa vipaumbele vya kisekta na badala yake kuwa na vipaumbele vya hatua za kiutekelezaji, ukibainisha kwa kina programu na shughuli za utekelezaji

Sifa Mahsusi za Mpango, inaendelea…

- Msukumo unawekwa zaidi katika ukuaji wa uchumi, pasipo kusahau kulinda mafanikio yaliyopatikana katika upatikanaji wa huduma za jamii, sawia na kulenga kuboresha rasilimali watu hususan kuendeleza ujuzi.
- Kuongeza nafasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi, kwa kuboresha mazingira ya biashara na kuwa na ufanisi katika matumizi ya nyezo za uzalishaji

3.0 MAHITAJI YA MSINGI YA MPANGO

Misingi minne (4):

- Kuendeleza utulivu wa uchumi(sera bora za fedha na bajeti)
- Mazingira na mabadiliko ya tabia nchi (sera, mikakati na mifumo bora ya kupunguza athari hizo)
- Utawala bora unaozingatia sheria (kuboresha sheria na mifumo ya kitaasisi, kutekeleza mradi wa vitambulisho vya Taifa)
- Ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi (kupima ardhi, kutoa hati na ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu kwa ajili ya makazi mijini na vijijini)

4.0 VIPAUMBELE VYA MPANGO

Vipaumbele vitano (5):

- **Miundombinu:** Kuwezesha kuondoa vikwazo katika uchumi. Maeneo ya mpango ni;
  - Nishati
  - Bandari
  - Reli
  - Barabara
  - Viwanja vya ndege/usafiri wa anga
  - Maji na usafi wa mazingira
  - Mawasiliano

Vipaumbele vya Mpango, inaendelea…

- **Kilimo:** kuwezesha kuinua tija na kuwanufaisha wananchi wengi

  wa vijijini. Maeneo ya mpango ni;

  - Mazao (uzalishaji na uthamanishaji)
  - Uvuzi (uzalishaji, soko na utafiti)
  - Misitu (uzalishaji na utunzaji)
  - Mifugo (uzalishaji, soko na utafiti)

Vipaumbele vya Mpango, inaendelea…

- **Viwanda:** Kuwezesha kuongeza thamani ya bidhaa, soko, ajira na Mapato. Maeneo ya mpango ni:
  - ➢Viwanda vya kati na vikubwa
  - ➢Kuanzisha kanda maalum za kiuchumi (SEZ and EPZ)
  - ➢Madini hususan katika kuongeza thamani ya madini na ushiriki wa wananchi

Vipaumbele vya Mpango, inaendelea…

- **Rasilimali Watu**

  - ➢ Kuboresha elimu na ujuzi ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira
  - ➢ Kuboresha mfumo na huduma ya afya katika ngazi zote

- **Utalii, Biashara na Huduma za Fedha**

  - ➢ Kukuza utalii, biashara na huduma za fedha ili kuchochea ukuaji wa uchumi

5.0 MAENEO YA UWEKEZAJI YA MPANGO

Maeneo Kumi (10) ya Uwekezaji:

- Uzalishaji wa umeme kufikia megawati 2780 MW
- Kuongeza uwezo wa bandari ya Dar es salaam
- Ukarabati wa reli ya kati na kuongeza idadi ya mabehewa na vichwa vya treni
- Ujenzi wa barabara za mikoa na wilaya katika ukanda wa kilimo wa kusini (SAGCOT)
- Miundombinu ya umwagiliaji katika ukanda wa kilimo cha Kusini (SAGCOT)

Maeneo ya Uwekezaji ya Mpango, inaendelea…

- Kusambaza mkongo wa Taifa wa TEHAMA nchi nzima
- Elimu ya sayansi, uhandisi na elimu kwa ujumla
- Kuendeleza maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ's) hasa kwa bidhaa za elektroniki, mitambo ya kilimo na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na madini
- Viwanda vikubwa vya kuzalisha mbolea
- Viwanda vya makaa ya umeme na chuma

6.0 UGHARAMIAJI WA MPANGO

- Gharama za kutekeleza mpango (2011/12 – 2015/16) ni Tsh 43.25 Trilioni (wastani wa Tsh 8.6 trilioni kwa mwaka)
- Mchango wa Serikali unakadiriwa kuwa Tsh. 2.7 trilioni kwa mwaka. Mchango wa Serikali katika bajeti ya maendeleo ni wastani wa Tsh. 1 trilioni kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Hivyo, ni muhimu ukusanyaji wa mapato ya ndani ukaimarishwa

Ugharamiaji wa Mpango, inaendelea…

- Mchango wa Serikali utatokana na vyanzo asili, na vyanzo mbadala ikiwa ni pamoja na kodi kwenye biashara za kifedha, "*Sovereign Bonds*", kodi kwenye faida kubwa za makampuni ya madini, "*Sovereign Wealth Funds*", mifuko ya ushirikiano kama vile China-Africa, India-Afrika, TICAD n.k.
- Mchango wa kiasi kilichobaki kinatarajiwa kitokane na mikopo, ubia na sekta binafsi,AZIKE, wahisani na nguvu za wananchi.

Ugharamiaji wa Mpango, inaendelea…

Makadirio ya Gharama

Sekta	Gharama (Tshs. T'rn)	Asilimia
1. Miundombinu	26.91	62.6%
Miundombinu (msingi)	*25.37*	*59.0%*
Miundombinu (mawasiliano)	*1.54*	*3.6%*
2. Kilimo	3.87	9.0%
3. Viwanda	3.01	7.0%
4. Maji	2.36	5.5%
5. Maendeleo ya Rasilimali Watu	4.57	10.6%
6. Mengineyo	2.53	5.3%
Jumla:	**43.25**	**100%**

7.0 MPANGO NA PROGRAMME NYINGINE ZA KITAIFA

- Mpango umejengwa juu ya malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, MKUKUTA II, mipango ya kisekta, mikoa na wilaya. Mpango unajumuisha nguvu za wadau wote (Serikali, nguvu za wananchi, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, wafadhili, AZISE n.k.)

- Mpango ni awamu ya Kwanza ya Mpango Elekezi *("roadmap")* wa Miaka 15 ya kutekeleza Dira 2025 kwa utaratibu *("systematically")* ukiwa na viashiria vya kupima mafanikio *("specific indicators of progress"*). Lengo ni kuharakisha utekelezaji wa Dira 2025;

Mpango na Programme, inaendelea…

- Mpango unajielekeza zaidi kuongeza ukuaji uchumi-tajirishi *("wealth-creating growth")* kwa kujielekeza kuvunja vikwazo vya kukuza uchumi nchini.
- Mipango na mikakati mingine ya kitaifa ikiwemo MKUKUTA II na sekta, mikoa na wilaya inakusudiwa kuendana na mpango wa maendeleo ili kufikia malengo ya Dira 2025

8.0 MFUMO WA UTEKELEZAJI

- Wizara na Mikoa zitawajibika kusimamia na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango
- Wizara na Mikoa zitawajibika kuwashirikisha Wadau na Wananchi katika kuibua fursa na maeneo ya kuchangia katika kutekeleza mpango
- Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itawajibika kutathmini, kufuatilia na kuandaa taarifa ya miradi ya mpango

Mfumo wa Utekelezaji, inaendelea…



9.0 MPANGILIO WA VIASHIRIA VYA MALENGO YA DIRA 2025 KATIKA MPANGO (2011/12 – 2015/16)

Lengo	Mwaka 2010	Mwaka 2015
Pato la Mtanzania	$ 500 (2009)	$ 670
Pato la Taifa	6.5%	8.0%
Kiwango cha ukuaji wa kilimo	4.6%	6.0%
Kiwango cha ukuaji wa viwanda	7.0%	8.2%
Kiwango cha ukuaji wa huduma	7.2%	7.5%
Kiwango cha ukuaji mauzo nje	8.4%	10.0%
Kiwango cha misaada	13.7%	10.0%
Umeme	81.7 Kwh	200 Kwh
Mapato (% ya Pato la Taifa)	17.5%	19.0%

10.0 HITIMISHO

Wajibu wa Wadau:

- **Serikali:** Kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kutekeleza mpango
- **Wizara na Mikoa:** Kuchangia katika kuibua fursa na kusimamia utekelezaji wa mpango
- **Sekta Binafsi na AZIKE:** Kuchangia katika kufanikisha mpango (fedha na utaalum)

Hitimisho, inaendelea…

- **Washirika wa Maendeleo:** Kujaza pengo katika rasilimali (fedha na utaalum) zinazohitajika kutekeleza mpango

- **Wananchi:** Kuchangia katika kuibua fursa na kushiriki kwa bidii, juhudi na maarifa katika kutekeleza mpango

“PENYE NIA PANA NJIA”
TANZANIA KUWA NCHI YENYE HADHI YA KIPATO CHA KATI IFIKAPO 2025 INAWEZEKANA

ASANTE SANA

THANK YOU